REPUBLIC OF KENYA

# WIZARA YA ELIMU

# HATI YA UTOAJI HUDUMA KWA UMMA

MAONO: ELIMU BORA, INAYOFAA NA SHIRIKISHI, MAFUNZO NA UTAFITI
MAARUBU: KUTOA, KUIMARISHA NA KUSHIRIKISHA UTOAJI ELIMU YENYE MANUFAA NA USAWA, MAFUNZO NA UTAFITI KWA MAENDELEO ENDELEVU

| NAMBARI | HUDUMA | MAHITAJI YA MTEJA | GHARAMA YA BIDHAA AU HUDUMA (endapo itahitajika) | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kujibu Barua | Barua (Iliyochapishwa au barua pepe) | Hakuna malipo | Katika muda wa siku tano za kikazi |
| 2. | Usajili wa shule za umma za elimu ya msingi, shule za binafsi na vyuo vya mafunzo | Barua ya maombi: Kumbukumbu za kikao cha bodi ya elimu kwenye kaunti: taarifa za kuthibitisha viwango na utathmini wa viwango: ripoti ya hali ya afya ya umma; Ripoti ya halmashauri ya NEMA (Iwapo itahitajika) nakala ya cheti cha kumiliki au kodisha ardhi; Mchoro wa shule; rekodi za viwango vya elimu vya walimu. | Shule za elimu msingi za umma na vyuo vya umma- shilingi elfu mbili (2,000/) Shule za upili za binafsi na vyuo vya mafunzo vya binafsi Shilingi elfu kumi (10,000) | Siku 30 za kikazi tangu kupokea maombi |
| 3. | (a) Usambazaji wa fedha za kufadhili elimu ya msingi, sekondari msingi,elimu ya upili bila malipo katika shule za kutwa na hazina ya masomo | Cheti cha usajili wa shule, takwimu kuhusu usajili wa wanafunzi kwenye mfumo wa usimamizi wa elimu (KEMIS); taarifa sahihi ya nambari ya akaunti ya benki, Mintaarafu ya kikao cha bodi ya usimamizi, nakala ya barua ya uteuzi wa mwalimu mkuu/ msimamizi na tume ya TSC. | Bila malipo | Siku 7 baada ya kupokea taarifa ya kifedha |
| | (b) Usambazaji wa fedha za kufadhili masomo ya wanafunzi, na ruzuku kwa vyuo vya mafunzo ya kiufundi | Taarifa sahihi za akaunti za benki za vyuo, taarifa ya usajili wa wanafunzi. | Bila malipo | Siku 14 baada ya kupokea taarifa ya kifedha |
| | (c) Usambazaji wa fedha za ustawishaji na ulipaji mishahara katika vyuo vya mafunzo ya walimu | Taarifa sahihi kuhusu akaunti za benki za vyuo. | Bila malipo | Siku 14 baada ya kupokea taarifa ya kifedha |
| 4. | Uteuzi na usajili wa walimu wa Stashahada ya juu katika shule za msingi (DPTE) na Stashahada katika elimu ya chekechea (DECTE) | Cheti cha P1 au ECDE | Bila malipo | Siku 30 za kikazi |
| 5. | Uteuzi na usajili wa walimu kwa mafunzo ya stashahada katika elimu maalum (SNE) | Fomu ya maombi iliyoidhinishwa, Awe na umri wa chini ya miaka 50 Awe mwalimu aliyeajiriwa na tume ya TSC na kuhudumu kwa aghalabu miaka 5; Awe na cheti cha P1, DPTE na awe raia wa Kenya. | Bila malipo | Siku 30 za kikazi |
| 6. | Uteuzi wa bodi za usimamizi wa elimu katika kaunti katika taasisi za masomo ya msingi | Orodha za walioteuliwa na kumbukumbu za mikutano, wasifu Kazi wa walioteuliwa; kumbukumbu za vikao vya uteuzi, kumbukumbu za mikutano ya bodi ya elimu kwenye kaunti, nakala za vitambulisho na vyeti vya masomo vya walioteuliwa. | Bila malipo | Siku 30 za kikazi |
| 7. | Uteuzi wa wenye viti na wanachama huru wa mabaraza ya vyuo vikuu na mabewa ya vyuo vikuu pamoja na wanachama wa bodi za mashirika ya serikali yaliyo chini ya wizara ya elimu | Barua za maombi, nakala za stakabadhi za masomo, wasifu kazi, nakala za vitambulisho au pasipoti. | Bila malipo | Siku 60 baada ya tangazo la nafasi hizo/kukamilika kwa muda wa kuhudumu kwa wanaoshikilia nafasi hizo. |
| 8. | Uteuzi wa Bodi za wasimamizi/ mabaraza ya vyuo vya kiufundi TVET | Kumbukumbu za jopo la uteuzi, wasifu kazi wa walioteuliwa. | Bila malipo | Siku 90 za kikazi |
| 9. | Uidhinishaji wa Stakabadhi za Kimasomo | Vyeti asilia na stakabadhi za kuvithibitisha; cheti cha kukamilisha masomo, taarifa za matokeo ya mitihani (ikiwa itahitajika) barua ya uidhinishaji, nakala ya pasipoti, nakala za vyeti asilia. | Bila malipo | Siku 3 |
| 10. | Uidhinishaji wa wanafunzi na wasaidizi wa wanafunzi walio na mahitaji maalum kusafiri nje ya nchi | Ombi lililoandikwa na shule; Orodha ya wanafunzi wanaosafiri; Orodha ya walimu watakaoandamana na wanafunzi; Idhini ya wazazi wote wawili; Nakala ya kitambulisho cha angalau mzazi mmoja; Agizo la mahakama iwapo kuna mlezi; Ushahidi wa ufadhili wa masomo; Nakala ya pasipoti ya mwanafunzi; Barua ya mwaliko kutoka kwa taifa alishi, Bima za matibabu na usafiri; Nakala ya bima ya gari au magari. | Bila malipo | Siku 7 za kikazi |
| 11. | Utoaji wa vyeti vya kuhitimu kwa wanafunzi watu wazima | Fanya mtihani kuthibitisha ustadii | Bila malipo | Siku 30 za kikazi |
| 12. | Matangazo na utoaji ufadhili wa elimu katika ngazi za kimataifa | Kutuma maombi mitandaoni (Katika baadhi ya mataifa ). Jaza fomu ya maombi wakati tangazo linapotolewa, Jitokeze kwa usajili unapoorodheshwa (utafahamishwa kupitia simu, ujumbe mfupi au barua pepe). Subiri kusajiliwa iwapo utateuliwa (Angalia barua pepe kuhusu uteuzi na mahojiano ya kimtandaoni iwapo itahitajika) | Bila malipo | Siku 21 za kikazi baada ya makataa ya kutuma maombi kukamilika. |
| 13. | Kuidhinisha wanafunzi wanaokwenda kwa mafunzo katika mataifa ya nje | Jaza fomu ya kuidhinishwa ( hati ya kiapo kuhusu ufadhili na taarifa kuhusu mwanafunzi ); Barua ya kusajiliwa; taarifa ya Benki; Vyeti vya masomo; Cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha kitaifa(ID); Kitambulisho cha mdhamini; Picha ya paspoti ya mwanafunzi; Barua ya kukamilisha kulipa mkopo wa bodi ya utoaji mikopo ya elimu ya juu (HELB). | Bila malipo | Siku 1 |
| 14. | Utoaji habari sahihi na muhimu kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu kwa njia inayorahisisha upatikanaji wa habari | Ombi lililoandikwa | Bila malipo | Siku 7 |
| 15. | Kukuza na kutangaza tuzo, zawadi na ufadhili katika yanja za sayansi, teknolojia na ubunifu | Matangazo na maombi yaliyoandikwa | Bila malipo | Siku 7 |
| 16. | Utoaji ushauri wa kitaalamu na nasaha kuhusu STI | Ombi lililoandikwa | Bila malipo | Siku 2 |

***TUMEJITOLEA KWA HESHIMA NA UBORA KATIKA UTOAJI HUDUMA***

Kwa huduma au bidhaa zozote zinazotolewa bila kuzingatia viwango vilivyoorodhershwa au afisa yeyote atakayekosa kuwajibikia heshima na ubora katika utoaji huduma, piga ripoti kwa:


Waziri wa Elimu
Wizara ya Elimu,
Simu: +254(0)02033185/331858
Barua Pepe: info@education.go.ke
Jogoo House "B" Taifa Road
S.L.P 300400-00100, Nairobi.

Katibu wa Tume/ Afisa Mkuu Mtendaji,
Tume ya Utekelezaji Haki,
2nd Floor, West End Towers, Waiyaki Way,
Nairobi.
S.L.P 20414-00200 Nairobi
Simu: +254(0)202270000/2303000
Barua Pepe: complain@ombudsman.go.ke


***HUDUMA BORA NI HAKI YAKO***